

# HALMASHAURI YA WILAYA MASASI

## “TANGAZO”

### MAMBO MUHIMU KATIKA KUPAMBANA NA CORONA

1. Nawa mikono na sabuni mara kwa mara.
2. Hakikisha haugusigusi usoni, puani, mdomoni na machoni ambayo ndiyo milango mikuu ya CORONA kuingia mwilini.
3. Ziba midomo na pua unapokohowa kwa kutumia Leso, Tissue, n.k.
4. Vaa maski kuziba mdomo na pua unapokuwa karibu na mikusanyiko.
5. Kama hauumwi sio lazima kuvaa maski, labda kama unatoa huduma kwa mshukiwa wa ugonjwa wa CORONA.
6. Kaa umbali wa mita moja toka kwa mtu anayekohowa.
7. Safisha vitu vinavyoguswa mara kwa mara kama vile meza, vitasa, mlango, swichi za umeme, simu, vyoo, masinki na vingine vinavyofanana na hivyo.
8. Epuka mikusanyiko yote isiyokuwa ya lazima na kila mmoja asambaze ujumbe kwamba mikusanyiko imepigwa marufuku hadi itakapoelekezwa vinginevyo. Mikusanyiko hiyo ni kama Pulltable, karata, draft, bao, michezo ya watoto rede, football, vibanda vinavyoonesha Video.
9. Acha/Sitisha safari zisizo za lazima.
10. Fuata maelekezo yanayotolewa na serikali kupitia viongozi na wataalam wa Afya.

Imetolewa na,



Gabriel K. Joshua

KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI (W)  
MASASI

KAIMU MKURUGENZI  
HALMASHAURI YA WILAYA  
S. L. P. 60, MASASI